Wale ambao huweka msingi wao wa huruma juu ya ufahamu wa tafakari isiyo ya pande mbili
Wale ambao moyo wao umetulia na Upendo wa Mungu kwa “mpendwa jirani...”
Wale wanaowaambia ukweli wenye nguvu...

**WIMBO:** Damu ya Kristo, utukomboe!

## TUSALI KWA AJILI YA ...

Wale wanaofanya kazi kwa ajili ya kutetea haki...
Wale wanaowatembelea wale waliowatendea vibaya...
Wale wanaowatunza wagonjwa na wazee ...
Wale wenye kuupenda kwa moyo Ulimwengu wetu ...
Wale wanaofanya kazi ya kupinga ubaguzi wa rangi...
Wale ambao hutumikia nchi zao vizuri...

**WIMBO:** Damu ya Kristo, utukomboe!

Wale ambao wana changamoto na kufanya kazi kubadili mifumo na sheria zisizo za haki ...
Wale ambao ni uwepo wa huruma kwa watu na katika hali ...
Wale ambao hutoa maisha yao katika huduma ya dada na kaka zao ...
Wale ambao hulisha wagonjwa na wale ambao wanahitaji afya na uadilifu ...
Wale wanaoishi Injili ya Yesu ...
Wale ambao ... (kwa hiari ...)

**WIMBO:** Damu ya Kristo, utukomboe!

**TUSALI KWA PAMOJA...** Baba yetu...

**WIMBO:** **WIMBO WA DAMU YA KRISTO**

# SALA KWA AJILI YA SHEREHE YA DAMU AZIZI

Usifiwe na ubarikiwe Moyo Mtakatifu na Damu Azizi ya Yesu katika Sakramenti Takatifu ya Altare, sasa na hata milele. Amina.

**WIMBO:** Damu ya Kristo, utukomboe

**SOMO:** Waefeso 2, 13-18

## LITANIA YA DAMU YA KRISTO

(kusali aya zifuatazo mmoja mmoja kwa uhuru au kupokezana watu wawili – taratibu na kwa tafakari)

Damu ya Kristo, iliyomwagika ulipotahiriwa, iwabariki wale wote wanaodhulumiwa kingono na wanaobakwa, makahaba, waathiriwa na familia za wale waliodhulumiwa na Mapadri na Maaskofu, na wale wote ambao wameangukia katika mtandao wa usafirishaji haramu wa binadamu.

Damu ya Kristo, iliyomwagika kwa uchungu katika bustani ya Gethsemane, iwabariki wale wote wanaoteseka kutokana na uchaguzi na maamuzi yaliyofanywa ili kuendelea kuwa waaminifu kwako; iwabariki mashahidi wa leo, wale ambao wanajitahidi kubaki waaminifu kwako wakati wa mateso na pia wale waliotoa Uhai wao.

Damu ya Kristo iliyomwagika ulipopigwa mijeledi, iwabariki wale wote waliomkosea Mungu, waliojikosea wao wenyewe, waliowakosea wengine pamoja na viumbe, uwajaze amani ambayo ni zawadi ya msamaha wako.

Damu ya Kristo, iliyomwagika ulipotiwa taji la miiba, iwabariki wote ambao katika ulimwengu wetu wanabaguliwa kwa sababu ya kabila, dini, ngono au nchi ya asili.

Damu ya Kristo, iliyomwagika kwenye njia ya Kalvari, itufundishe kutembea pamoja kwa Amani ili tuweze kupata namna ya kuishi kwa usawa na heshima kwa utu wa watu wote katika kila kona ya Ulimwengu wetu.

Damu ya Kristo, iliyomwagika Msalabani, itufundishe kutoa Uhai kwa ajili ya wengine, kwa uhuru na kwa ukarimu. Mbele ya ukosefu wa haki, utupe ujasiri tuweze kuwasaidia wale wanaogandamizwa na wale wote wasio na sauti, pamoja na Maria Mama yako na Mama yetu.

Damu ya Kristo iliyomwagika toka pale ulipotobolewa iwabariki wale wote waliovunjika moyo kutokana na maumivu, woga, uonevu, unyanyasaji wa kijinsia wa wachungaji, kutoka katika huzuni yenye hamu ya kupata haki.

**WIMBO:** Damu ya Kristo, utukomboe

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika katika mataifa yaliyotengwa na machafuko ya silaha, ghasia, machafuko ya wenyewe kwa wenyewe, vita na vitisho: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika katika mauaji ya wasio na hatia, katika unyanyasaji wa watoto na wanawake na katika janga la ubaguzi wa rangi: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa wale wanaoilinda nchi, ardhi na mali: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa hofu na kukata tamaa kwa wahamiaji, wasio na makazi, wenye njaa na wasio na ajira: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa wazee waliosahaulika, waliotengwa, wanaodharauliwa au wanaokufa wakiwa peke yao: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa wakimbizi ambao hufika pwani bila kukaribishwa au wanaokufa njiani: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa wale ambao hawana nafasi ya kupata elimu au kuwa na kazi inayoaminika: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa wale waliotekwa nyara au kufungwa jela bila haki: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa wale wanaokufa peke yao, wasiohitajika, waliosahaulika na wasiopendwa: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa wale wanaoteseka kwa madawa ya kulevya na wanaougua maradhi ya aina yoyote ile: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa wale ambao wameuawa kwa ukatili wa mapolisi, na wale ambao wapo kwenye safu ya kifo au waliouawa "kisheria": utukomboe!

Damu ya Kristo ambayo bado inamwagika kwa wale ambao wanateseka kwa sababu ya Virusi vya Korona na magonjwa mengine yote, ya kimwili, ya Kisaikolojia, ya kihisia na ya kiroho, na kwa wale ambao wanawatunza. Utukomboe!

Damu ya Kristo ambayo bado inamwagika katika unyonyaji na matumizi yasiyofaa ya ardhi na rasilimali zake na katika kutoweka kwa aina nyingi ya viumbe hai. Utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa sababu ya sheria zisizo halali na wabunge ambao wanapendelea matajiri na kuwakandamiza maskini: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa moto, mafuriko na hali mbaya ya hewa: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kupitia ongezeko la joto ulimwenguni na athari zake zote: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa kaka na dada zetu, na wanyama pori wanaokufa kwa njaa na kiu: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwenye mito, baharini na hewa iliyochafuliwa: utukomboe!

Damu ya Kristo, ambayo bado inamwagika kwa ubinafsi wa wale wanaopata fursa na nguvu ya kukuza udhalimu na ukosefu wa usawa: utukomboe!

**WIMBO:** Damu ya Kristo, utukomboe!

**TAFAKARI KATIKA UKIMYA** (dakika 5-10)

**KUSHIRIKISHANA:**

1. Je! Ni hali gani tuliyoiombea ambayo imegusa moyo wako?
2. Ni hali gani ambazo hazikutajwa kwenye Litania?
3. Moyo wako unavutwa wapi?
4. Utafanya nini kama mtu binafsi?
5. Mtafanya nini kama Jumuiya?

**WIMBO:** Damu ya Kristo, utukomboe!

**TUSALI KWA AJILI YA...**

Wale ambao wako upande wa ...
Wale ambao wanazungumza kwa ........
Wale ambao hutoa hifadhi....
Wale wanaowalisha wenye njaa...
Wale wanaowanywesha wenye kiu...
Wale wanaotafuta Amani kwa ajili ya wote...

**WIMBO:** Damu ya Kristo, utukomboe!

Wale wanaoishi katika amani...
Wale wanaokusanya taka na kuzitumia...
Wale wanaowakaribisha wageni...